

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini

SAUTI YA MTUMIAJI

Toleo Na.01 Machi – Mei, 2021



Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA Consumer Consultative Council), lipo kwa mujibu wa kifungu namba 29 cha Sheria namba 3 ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, (LATRA) ya Mwaka 2019. Sheria ya LATRA imefuta iliyokuwa Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). Sheria hiyo ilianza rasmi kutumika Tarehe 29 Aprili, 2019, baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali (GN.No. 358) la tarehe 26/04/2019.

Baraza ni Chombo cha Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini. Limepewa dhamana ya kuwakilisha na kutetea maslahi na haki za Watumiaji wa huduma za Usafiri Ardhini.

Majukumu ya Baraza ni:

- (i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini, kwa kuwasilisha, kupata maoni na taarifa na kwa kushauriana na Mamlaka, Waziri mwenye dhamana na wadau wa sekta mbalimbali zinazodhibitiwa;
- (ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni mbalimbali kuhusu masuala yanayowagusa watumiaji wa huduma zinazosimamiwa na LATRA;
- (iii) Kuunda kamati za Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Sekta zinazodhibitiwa na LATRA katika Mikoa na kushauriana nazo;
- (iv) Kushauriana na wadau , Serikali na makundi ya watumiaji kuhusu huduma;

- (v) Kuunda mabaraza ya Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini, kwenye maeneo ya Jamii na Kushauriana nazo;
- (vi) Kufanya utafiti juu ya maslahi, haki, wajibu na masuala mengine yanayogusa watumiaji.

Dira ya Baraza

Ni kuwa Baraza bora kikanda katika kuwezesha na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri Ardhini.

Lengo Kuu la Baraza

Ni kukuza na kulinda maslahi ya watumiaji ili kupata uwakilishi na mwitikio mpana kwa mdhibiti, watunga sera na mtoa huduma ya usafiri Adhini.

Kukamilisha Uongozi wa Baraza.

Baada ya Mh. Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, kukamilisha uteuzi wa Wajumbe wa Baraza, Wajumbe hukutana na kuchagua miongoni mwao, mwenyekiti wa kuliongoza Baraza hilo kwa kipindi cha miaka mitatu, hii ni kwa mujibu wa Kifungu namba 29 (7) cha Sheria namba 3 ya LATRA ya Mwaka 2019. Utekelezaji wa kifungu hiki ulifanyika tarehe 19 Aprili, 2021 katika ukumbi uliopo ghorofa ya 27 Jengo la TPA, chini ya msimamizi wa uchaguzi huo Bw. Gabriel Migire, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi – Uchukuzi. Wageni waalikwa walioshuhudia uchaguzi huo ni Mkurugenzi Mkuu LATRA Bw. Gilliard W. Ngewe na Mkurugenzi wa Fedha na Raslimali Watu LATRA Bw. Samwel D. Keenja. Angalia picha hapa chini.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi- Uchukuzi, Bw. Gabriel J. Migire, akiwa na Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini, wakati wa Kikao cha kuchagua Mwenyekiti wa Baraza. Kulia kwake ni Dr. George Makuke, aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza hilo kwa kipindi cha miaka mitatu (03) kuanzia tarehe 26 Februari, 2021. Kushoto kwake ni Bw. Leo John Ngowi, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza. Wengine waliosimama kuanzia Kulia ni Bi. Fatuma Kulita (Sekretarieti), Bw. Ebenezer S. Mshana (Mjumbe) Bw. Said H. Putta (Mjumbe) Bw. Hassani R. Mnyone (mjumbe) Bw. Manyama M. Kanyere (Mjumbe) Bw. Gilliard W. Ngewe (DG LATRA) na Bw. Samwel D. Keenja (Ag. DFA – LATRA)

Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza.

1. Elimu na uhamasishaji

Katika kutekeleza majukumu ya Baraza LATRA CCC, ilitoa elimu kwenye kituo Kikuu cha Mabasi ya Masafa Marefu cha JPM kilichopo Mbezi Luis. Elimu ilitolewa, pamoja na kugawa vipeperushi kwa abiria mbalimbali.

- (i) Elimu juu ya Abiria kujikinga na Maambukizi ya COVID 19 kwenye Vyombo vya Usafiri wa Umma. Elimu ilitolewa kwa kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya.
- (ii) Elimu juu ya Abiria kukata tiketi kwa njia ya mtandao;
- (iii) Kuhamasisha abiria wa Kituo Cha Mabasi cha Mbezi kupanda magari kwa kukaa kwenye Mstari.

Jedwali la utoaji wa elimu kwenye vituo vya mabasi, Radio, na TV

s/n		Chombo	Idadi	Idadi ya Wadau waliofikiwa
1	Idadi ya Programu za Uelimishaji zilizotolewa	TV	9	Jamii pana
		Radio	15	Jamii pana
		Magazeti	3	Jamii pana
2	Elimu kwenye Mabasi ya abiria kati ya 50- 60	Kituo cha mabasi	89	Zaidi ya abiria 4,000

Source: latra ccc Machi – Mei, 2021

Pia, elimu inatolewa, kwa njia ya mitandao ya kijamii kama Whatsapp, Instagram, tweeter, You-Tube na www.latracc.go.tz

2. Mafunzo kwa Wasioona.

Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Usafiri Ardhini, lilitoa mafunzo kwa wasioona juu ya ukataji tiketi kwa njia ya mtandao. Mafunzo yalifanyika tarehe 7 Mei, 2021 katika ukumbi wa mikutano uliopo Kituo cha Mabasi cha JPM Kilichopo Mbezi Luis. Mafunzo yalilenga kujenga uelewa kwa abiria, wasioona, kulifahamu LATRA CCC, kujua haki na wajibu wawapo kwenye vyombo vya usafiri na kukata tiketi kwa njia ya Mtandao.

Mafunzo, yalifunguliwa na Bi. Beatrice Mbawala aliyemwakilisha Mh. Mkuu wa Wilaya ya Ubungu, na yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo, Mwenyekiti wa LATRA CCC, Sekretarieti ya LATRA CCC, Viongozi wa Tanzania Associations of Blinds (TAB), Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Kituo cha Mabasi cha JPM Mbezi Luis, Meneja wa Kituo cha JPM, Wasioona zaidi ya 50, na Waandishi wa habari.



Mwenyekiti wa LATRA CCC Dr. George Munubhi Makuke, wa pili kushoto akitoa maneno machache kwa Washiriki na kumkaribisha Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Ubungu, ili afungue mafunzo kwa wasioona.

Wakati wa Ufunguzi wa Mafunzo, Bi. Beatrice Mbawala aliwajulisha washiriki kuwa, tafiti nyingi zinaonyesha kuwa, nchi nyingi zilizosonga mbele katika maendeleo ya Uchumi, ni zile zinazotumia mifumo madhubuti ya kiteknolojia na kuwa na kumbukumbu sahihi kwa ajili ya mipango endelevu ya mataifa hayo. Nasi Tanzania hatunabudi kuhamasishana na kuwa na Azma moja ya kutumia teknolojia iliyopo hivi sasa ya ukataji tiketi kwa njia ya Mtandao.

Alieleza kuwa, Mfumo wa Tiketi Mtandao umetengenezwa kwa kuzingatia mahitaji mbalimbali ya Abiria, Wamiliki wa Mabasi na Serikali kwa:

- i. Kurahisisha maisha ya abiria wetu katika ukataji wa tiketi na kufanya malipo bila kulanguliwa hususan kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka;
- ii. Kuzingatia na kurahisisha mahitaji ya abiria wasio na simu janja
- iii. Mfumo utatatua changamoto nyingi katika Sekta yetu ya Usafiri wa Abiria

Faida kwa abiria

- Kuokoa muda na gharama za kwenda kukata tiketi kwenye vituo vya mabasi.
- Kuepuka usumbufu wa kukata tiketi katika vituo vya mabasi.
- Kuepuka adha ya upandishwaji wa nauli holela /ulanguzi
- Kupata basi ambalo ni chaguo lake
- Kuwa na uhakika wa kupata nafasi (siti) kwenye basi siku ya safari.
- Atakuwa na kumbukumbu ya kudumu kuhusu safari yake

Faida kwa wamiliki wa mabasi

- Kupata fedha zao kiurahisi
- Kuondokana na uvujaji wa makusanyo
- kuwa na kumbukumbu ya kudumu kwa abiria wote wanaosafiri.
- Kupunguza gharama za uendeshaji.
- Kukopesheka kwa urahisi kutokana na taarifa za fedha kuwa bayana
- Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa biashara yake

- Kuwa na taarifa ya idadi ya abiria kwenye mabasi yake muda wowote

Faida kwa serikali

- Kupata takwimu sahihi na za kutosha zinazohusiana na sekta za usafirishaji.
- Kuiwezesha serikali kutambua maeneo yenye kipaumbele cha Ujenzi wa Miundombinu na uwekezaji wa huduma za usafiri.



Bi. Beatrice Mbawala, akitoa hotuba fupi, wakati wa ufunguzi wa Mafunzo kwa wasioona. Alisisitiza washiriki wote wajifunze kwa bidii, na watumie fursa hii kujua haki na wajibu wao wawapo kwenye vyombo vya usafiri Nchini.



Aliyesimama ni Bw. Omari Kiongo Itambu Mwenyekiti wa The Blind Association of Tanzania (TAB), akimshukuru muwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo kwa kutambua umuhimu wao katika Sekta ya Uchukuzi. Bw. Kiongo ni Mwenyekiti na Mkufunzi wa maandishi ya nukta nundu. Alimhakikishia muwakilishi wa Mkuu wa Wilaya kuwa watajifunza kwa bidii na wataendeleza elimu waliyoipata kwa makundi mbalimbali Nchini kwani wao wanauwezo mkubwa wa kusoma na kuelimisha watu wengine na watu wa Rika Tofauti. Aliomba Serikali iwasaidie vitendea kazi ili kazi isongo mbele.



Kondakta ya Kampuni ya ABC akionyesha kifaa kiitwacho Point of Sell (POS) wakati Mafunzo yakiendelea



Washiriki wakisikiliza Mafunzo kwa makini.



Picha ya Pamoja ya Washiriki wa Mafunzo ya ukataji tiketi kwa njia ya Mtandao.

Malengo na Matarajio zaidi ya Baraza kwa mwaka wa Fedha 2021/22

1. Kuhimiza zaidi matumizi ya tiketi mtandao na Smart Cards kwa mabasi ya Mijini.
2. Kuhamasisha Abiria Kupanda mabasi ya Mijini kwa mstari.

Malengo ya Azma hii ni pamoja na:

- (a) Abiria wa kwanza kufika kwenye kituo kuwa wakwanza kupata huduma ya usafiri kiustaarabu
- (b) Kuwawezesha watoto, wazee, akina mama wajawazito, wagonjwa na abiria wote kupata huduma stahiki kwa wakati
- (c) Kujenga jamii iliyostaarabika;
- (d) Kuponya majeraha ya muda mrefu ya abiria kuteseka vituoni
- (e) Kutunza vyombo vya usafiri (Milango na madirisha)

- (f) Kuepusha ajali na majeraha ya mwili, kupunguza uwezekano wa maambukizi ya magonjwa
- (g) Kuongeza utu, umoja, upendo, mshikamano katika jamii ya wasafiri.